

102/3  
KISWAHILI  
FASIHI  
KARATASI YA TATU  
JULAI / AGOSTI 2014  
MUDA: SAA 2½

## MTIHANI WA MWIGO WA WILAYA YA KURIA MASHARIKI 2014

Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Kidato cha Nne Nchini Kenya  
KISWAHILI  
FASIHI  
KARATASI YA TATU  
MUDA: 2 ½

### MAAGIZO

1. Jibu maswali manne pekee.
2. Swali la kwanza ni la lazima.
3. Usijibu maswali mawili kutoka kwa kitabu kimoja.

Karatasi hii ina kurasa 4 zilizopigwa chapa. Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yamo.

## **SEHEMU YA A: TAMTHILIA (SWALI LA LAZIMA)**

### **MSTAHIKI MEYA: Timothy Arege**

1. “Mchimba kisima huingia mwenyewe.” Kwa kurejelea jumuiya ya wanacheneo, thibitisha ukweli wa methali hii. (alama 20)

## **SEHEMU YA B: HADITHI FUPI**

### **DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE na Ken Walibora na Said A. Mohamed.**

#### **Jibu swali la 2 au la 3**

2. Eleza uozo unaokashifiwa katika hadithi zifuatazo katika diwani ya Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine.
- (a) Samaki wa nchi za joto. (alama 5)
  - (b) Damu Nyeusi. (alama 5)
  - (c) Kikaza (alama 5)
  - (d) Kanda la usufi. (alama 5)

**AU**

3. Kwa kurejelea hadithi zozote nne, kutoka kwa Diwani ya Damu Nyeusi na hadithi nyingine, thibitisha ukweli wa methali, “Mhini na mhiniwa njia yao ni moja.” (alama 20)

## **SEHEMU C: RIWAYA**

### **KIDAGAA KIMEMWOZEA na Ken Walibora.**

#### **Jibu swali la 4 au la 5**

4. “Umenena ndipo ndugu yangu. Hiyo ndiyo tanzia ya Afrika huru .....”
- (a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
  - (b) Ni sifa zipi za mvuto zinazowaleta pamoja mzungumzaji na mzungumziwa. (alama 4)
  - (c) Tambua na kufafanua mbinu iliyotumiwa katika dondoo hili. (alama 2)
  - (d) Kwa kutoa mifano, fafanua tanzia hiyo inayorejelewa katika dondoo. (alama 10)

5. Fafanua aina **tano** za migogoro inayojitokeza katika riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (alama 20)

**SEHEMU YA E – FASIHI SIMULIZI**

**Jibu swali la 6 au la 7**

6. Fafanua sifa na umuhimu wa malumbano ya utani katika jamii. (alama 20)

**AU**

7. Eleza umuhimu wa aina zifuatazo za nyimbo. (alama 20)

- (i) Hodiya
- (ii) Sifo
- (iii) Bembea
- (iv) Mbolezi

**SEHEMU YA D – FASIHI SIMULIZI**

8. **Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata:**

Nimeona, milima na mabonde, misitu na nyika.

Nimeona, majani na umande, uliotandazika.

Nimeona, mkulima yuwenda, shambani.

Nimeona, uwanda wa magugu, yalomkabili.

Nimeona, wajibu wa vurugu, 'wiano mkali.'

Nimeona, mkulima akiwa tayari.

Nimeona, kwa ari na juhudi, anatupa jembe.

Nimeona, kakaza ukaidi, kwa nguru achimbe.

Nimeona, mkulima akiwa kazini.

Nimeona, kijua kinawaka, kama jahanamu!

Nimeona, jembe kinuka, linapohujumu.

Nimeona, mkulima akiwa mbioni.

Nimeona, mvua yamiminika, naye hatohisi.  
Nimeona, kwa kani anatumka, bila wasiwasi.  
Nimeona, mkulima akiwa kazini.

Na sioni, jasho linapomwaika, yendapo mazao.  
Na sioni, haadhiye kutukuka, ila kilio.  
Kwa nini? Nauliza mkulima: kwani?

### **Maswali**

- (a) Eleza ujumbe muhimu katika shairi hili. (alama 4)
- (b) Dondoa na ueleze mfano mmoja wa uhuru wa mshairi. (alama 2)
- (c) Eleza mbinu za uandishi zilizotumika katika shairi hili. (alama 6)
- (d) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha nathari. (alama 4)
- (e) Ukirijelea shairi, onyesha umuhimu wa matumizi ya:
- (i) Kihisishi (alama 2)
- (ii) Kiulizi (alama 2)